



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA
BARAZA LA FAMASI



TAARIFA KWA UMMA

KUONGEZWA MUDA WA KUHUISHA TAARIFA ZA WANATAALUMA WA KADA YA FAMASI (RETENTION) KWA MWAKA 2025

DODOMA: 20 Januari 2025

Vifungu Na. 22, 26 na 30 vya Sheria ya Famasi, Sura 311 (The Pharmacy Act, Cap 311), vinaelekeza kuwa kila Mwanataaluma aliyesajiliwa, aliyeandikishwa au aliyeorodheshwa anatakiwa kuhuisha taarifa zake katika rejesta ya wanataaluma ya Baraza la Famasi kabla ya tarehe 31 Desemba ya kila mwaka.

Itakumbukwa kwamba tarehe 01 Desemba 2024 Ofisi ya Msajili ilifungua dirisha la kuhuisha taarifa na leseni za wanataaluma wa kada ya Famasi kwa mwaka 2025.

Kutokana na changamoto iliyojitokeza katika mfumo wa Baraza la Famasi (**Pharmacy Council Information Management System – PCMIS**) kushindwa kutoa ankara za malipo (*Control number*) ofisi ya Msajili inapenda kuwatangazia wanataaluma wa kada ya Famasi kuwa imeongeza muda wa kuhuisha taarifa na leseni mpaka tarehe **10 Februari 2025**.

Tunaomba radhi kwa usumbufu wowote uliojitokeza wakati wote changamoto hii ilipokuwa inashughulikiwa. Hivyo, tunawasihi wanataaluma kuendelea kuhuisha taarifa zao bila faini mpaka tarehe tajwa hapo juu.

Imetolewa na:

Msajili,
Baraza la Famasi,
S.L.P. 1277,
Dodoma

Simu: 0736222503/ 0736222516
Barua pepe: info@pc.go.tz /registration@pc.go.tz
Namba ya mawasiliano bila malipo 0800110015